Ardhi ya Kilimo Inapotea kwa Kasi Isiyotarajiwa: Eka 33,000... kila Siku!

Imeandikwa na Baher Kamal

Jangwa, madhara yanayoendelea kuletwa na hali ya ukame. Picha hii ni kwa hisani ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Mazingira (UNEP)

ROME, Agosti 16, 2016 (IPS) - Mwanadamu kila siku anashuhudia changamato mpya asizotarajia. Mojawapo ya changamoto hizi ni kwamba ardhi nyingi ya kilimo sasa inapotea kwa kiwango cha juu mno, kiwango ambacho hakijawahi kutokea katika historia ya mwanadamu cha mara 30 hadi 35. Kila mwaka, eka milioni 12 za kilimo zinapotea. Hii ina maana kwamba tunapoteza eka 33,000 kila siku!

Aidha, wanasayansi wamekadiria kwamba kiwango cha ardhi kinachokumbwa na ukame kimekua kwa asilimia 10-15 kuanzia miaka ya 1970 hadi zaidi ya asilimia 30 kufikia mwanzo wa miaka ya 2000, na takwimu hizi zinatarajiwa kukua katika siku zijazo.

Wakati ukame unaendelea kila mahali, Bara la Afrika linaonekana kama bara ambalo linaathiriwa zaidi na madhara ya ukame. Kulingana na Mkataba wa Bonn wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Uenezi wa Hali ya Jangwa (UNCCD), theluthi mbili ya ardhi ya nchi za Afrika sasa ni aidha jangwa au ardhi kavu.

Changamoto hii ni kubwa sana kwa bara hili la pili kwa ukubwa Ulimwenguni, ambalo watu bilioni 1.2 wanamoishi katika nchi 54, eneo ambalo limeathirika zaidi na tukio la hali ya anga la mwaka 2015/2016 linalojulikana kama mafuriko ya El-Niño.

Daniel Tsegai

IPS ilimhoji Tsegai, Afisa wa Programu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Uenezi wa Hali ya Jangwa (UNCCD), ambalo limeshirikiana na serikali ya Namibia katika maandalizi ya Mkutano wa Ukame Barani Afrika unaofanyika mnamo Agosti 15-19, Mjini Windhoek.

"Kimataifa, ukame unaendelea kuwa na athari mbaya zaidi, ukame unaendelea kutokea mara kwa mara, muda ambao ukame unatokea unaendelea kuongezeka na kwa ujumla uenezi wa kiwango kikubwa huku madhara yake yakiendelea kuongezeka. Madhara haya ni pamoja na idadi kubwa ya watu kuhama makazi yao na uhamiaji kwa kijumla. Hali ya sasa ya ukame unaoshuhudiwa ni ushahidi mwafaka. Mataifa mengi ya Afrika yameathirika vibaya sana, "Tsegai alifafanua.

Lengo la Mkutano wa Ukame Barani Afrika ni "kukumbana na hali ya ukame."

IPS iliuliza Tsegai kukumbana na hali ya ukame kunahusu nini? "Kukumbana na hali ya ukame kunafafanuliwa kama uwezo wa nchi kuhimili madhara makali ya ukame na kuweza kujikakamua kujikomboa kutokana na athari za baada ya ukame," Tsegei alieleza.

"Jambo la kwanza muhimu ni kufahamu sehemu nne za Ukame; Ukame wa Kimeterolojia (hali ya hewa), ukame wa Kihaidrologia (maji yaliyo ardhini), Ukame wa Kilimo na Ukame wa Kijamii na Kiuchumi (ambao huathiri wanadamu)."

Mambo Matano "Tunayokosa"

Tsegai alipoulizwa kama kuna changamoto kuu katika siku zijazo hasa katika suala la kukumbana na ukame barani Afrika, Tsegai aliambia IPS kuwa hizi ndizo changamoto kuu katika kukumbana na ukame:

a) Ukosefu wa data ya kutosha kama vile data ya hali ya anga, data ya vyanzo vya maji (maji ya juu ardhini na maji ya chini ardhini), data kuhusu unyevu wa udongo na pia data kuhusu matukio ya majanga ya ukame yaliyotendeka hapo awali na athari zake.

b) Uratibu duni miongoni mwa sekta mbalimbali husika na miongoni mwa wadau nchini na kati ya nchi katika kanda moja;

c) Kiwango cha chini cha uwezo wa kutekeleza hatua za kuzuia athari za ukame (hasa katika ngazi za chini);

d) Upungufu wa ari ya kisiasa ya kutekeleza sera za kitaifa za ukame, na

e) Uchumi wa maandalizi ya ukame ambao haujachunguzwa vyema, ili kuafikia uelewa mzuri wa manufaa ya kiuchumi yanayotokana na kufanya maandalizi kabla ya kipindi cha ukame.

Kulingana na malengo ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Uenezi wa Hali ya Jangwa (UNCCD), Tsegai anasema kwamba mataifa yanahitaji kutafuta njia za kuboresha uzalishaji wa ardhi na kuboresha hali za maisha za watu ambao wameathiriwa na ukame na kuenea kwa hali ya jangwa.

Kulingana na Tsegai, baadhi ya mikakati ambayo inaweza kuchukuliwa ili kujenga mbinu za kukumbana na jangwa ni pamoja na:

Kwanza: Mabadiliko ya jinsi tunavyoshughulikia ukame. Tutahitajika kubadilisha jinsi tunavyofikiria kuhusu ukame.

"Ukame kwa sasa sio tukio la wakati mmoja bali ni tukio la 'hatari'. Ukame utaendele kutokea muda baada ya muda, kutakuwa na vipindi vya ukame mkali mno na vinavyodumu kwa muda mrefu. Ni 'jambo la hatari' litakaloendelea kuwepo mara kwa mara, Tsegai aliambia IPS.

"Kwa hiyo, tunahitaji kusonga mbele na kuwa watu wenye vitendo bali sio watu wasio wa kutenda; kuanzia upande wa usimamizi wa hali za hatari; ambao unahitaji kuepuka njia chache zinazopendekezwa za kukumbana na ukame ambazo hazitumiki kufikia njia jumuishi za kimkakati za kukumbana na janga hili. Wazo la kulichukulia janga la ukame kama jambo la hatari kwa wanadamu lina maana ya kukumbana na dalili za ukame na sio visababishi vyake "Tsegai alielezea.

"Kwa kifupi, njia mwafaka ya kukumbana na ukame ni maandalizi ya kanuni za kitaifa zinazolenga ukame ambazo zinalingana na kanuni za upunguzaji wa hatari."

Pili: Kuimarisha Ufuatiliaji wa Ukame na mifumo ya kutoa onyo mapema (kuhusu ukame na madhara yake);

Tatu: Kutathmini uwezo wa nchi kukumbana na janga la ukame (Kuweka takwimu za ni nani anayeweza kuathirika zaidi na ukame, kwa nini? Je, ni eneo lipi litaathirika na madhara yake yatakuwa yepi?);

Nne: Kutekeleza mbinu za kihalisia za upunguzaji wa hatari za ukame ikiwa ni pamoja na maandalizi ya miradi ya umwagiliaji maji hasa kwa mimea na mifugo, ufuatiliaji na kupima vyanzo vya maji na matumizi ya maji, kujivunia njia zifaazo za kutumia tena maji na maji yaliyotumika kwa shughuli nyinginezo, kuchunguza uwezo wa kukuza mimea zaidi inayoweza kuhimili hali za ukame na kupanua bima ya mimea.'(/1}

Njia Tano za Kurekebisha Hali ya Ukame

Alipoulizwa ni nini matokeo ya Mkutano wa Ukame Barani Afrika, Tsegai alitoa majibu haya:.

1. Kuandaa Mkakati wa Afrika nzima, mkakati ambao utaimarisha maandalizi ya ukame barani Afrika ambayo yanaweza kutekelezwa na kushirikiwa katika kiwango cha nchi.
2. Kuongoza maendeleo ya sera jumuishi za ukame za kitaifa ambazo zinalenga kujenga jamii zaidi zinazoweza kukumbana na ukame kutokana na matumizi endelevu na usimamizi wa rasilimali za kiasilia (ardhi /udongo, misitu, viumbe hai, maji, nishati, nk).
3. Nchi zinatarajiwa kubuni Mkataba wa pamoja wa Ukame- kupitisha Azimio la Windhoek la Nchi za Afrika - ambalo litawasilishwa katika Mkutano wa Mazingira wa Mawaziri wa Nchi za Afrika mwaka ujao na azimio hili linatarajiwa kupitishwa na kikao cha Umoja wa Afrika.
4. Kwa kuzingatia haya, matokeo ya mkutano wa Windhoek yataleta majadiliano ya uidhinishaji wa matokeo ya mkutano miongoni mwa viongozi wa nchi na serikali za Afrika katika Umoja wa Afrika, na
5. Inatarajiwa kwamba mkutano utaimarisha urafiki na ushirikiano (Kusini - Kusini) ili kuunga mkono maendeleo ya sera mpya na mikakati ya kitaifa mpya na uboreshaji wa sera na mikakati iliyopo kuhusu usimamizi wa ukame.

Ukame, janga "lenye maafa makuu"

Imekadiriwa kwamba ukame ndilo janga la kimazingira lenye maafa makuu duniani na huathiri watu wengi zaidi kuliko janga lolote la kimazingira, Tsegai aliiambia IPS.

Kunao muda mdogo wa kuhakikisha kuwa watu milioni 23 wanaoishi katika hali za ukame Kusini mwa Bara la Afrika wanapokea msaada wa kilimo. | Picha ni kwa hisani ya: Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO)

"Ukame unazingatiwa kuwa na athari zaidi kuliko majanga yote ya kimazingira, huku ukisababisha madhara ya kiuchumi na kiekolojia ya muda mfupi na muda mrefu pia unasababisha athari zingine mbaya zaidi.

Tsegai anasisitiza kuwa ili kupunguza hali ya jamii kuathiriwa zaidi na ukame, mabadiliko ya mawazo kuhusu mbinu za usimamazi wa ukame yanahitaji kufanywa ili kukabiliana na mifumo iliyopo ya usimamizi wa ukame ambayo haitumiki na mbinu za usimamizi wa janga baada ya janga hilo kutokea. Kuwepo na mbinu tumikizi, mbinu za usimamizi wa majanga zinazolenga kushughulikia hatari zinazoletwa na janga hilo.

"Usimamizi wa ukame unaolenga hatari za ukame, hata hivyo, ni usimamizi unaojumuisha sehemu mbalimbali ambazo zinahitaji ujumuishaji wa wadau mbalimbali, na, kwa upande wa usimamizi wa sera ya ukame, usimamizi huu unahitaji uwezo wa wizara mbalimbali na taasisi mbalimbali za kitaifa kushirikishwa."